**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU

# WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA JANUARI, 2023

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU**

**UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA**

**KWANZA MWAKA 2023**

## 1.0 Utangulizi

**Ndugu Wanahabari;**

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii, kwanza kumshukuru **Mwenyezi Mungu** mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu mbalimbali tukiwa na afya njema.

**Pili**, Ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuwekeza katika Sekta ya Elimu kwa kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata fursa ya kupata elimu. Kutokana na uwekezaji huo, idadi ya Wanafunzi wanaojiunga Kidato cha Kwanza imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Chini ya uongozi wake, Wanafunzi wote wanaopata sifa ya kujiunga Kidato cha Kwanza wanapata nafasi bila ya kuwepo kwa Chaguo la Pili.

**Ndugu Wanahabari;**

Ikumbukwe kuwa mwaka 2021 Serikali ya Awamu ya Sita ilitoa Shilingi **Bilioni 240** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **12,000** katika shule za sekondari na kuwawezesha Wanafunzi wote **907,802** waliokuwa wamefaulu

kuanza masomo Januari, 2022. Vivyo hivyo kwa mwaka 2022, Mhe. Rais alipowasilishiwa makadirio ya ufaulu na kubaini kutakuwa na ongezeko la Wanafunzi, aliruhusu kutoa **Shilingi Bilioni 160** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **8,000.** Hivyo kama ilivyokuwa kwa mwaka 2021, mwaka huu pia hakutakuwa na Mwanafunzi atakayekosa nafasi katika Shule za Sekondari za Serikali ifikapo Januari, 2023. Nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu kupata nafasi ya kujiunga na Masomo ya Kidato cha kwanza **Januari 2023**.

## 2.0 Uchaguzi wa Wanafunzi Kujiunga na Kidato cha Kwanza Januari 2023

**Ndugu Wanahabari;**

Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Baraza la Mitihani la Tanzania imekamilisha Zoezi la Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka Januari, 2023. Uchaguzi ulihusisha wanafunzi **1,073,941** waliofaulu Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2022 waliotangazwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Kati yao, wavulana ni **514,846** na wasichana ni **559,095** ambao wote wanasifa stahiki ya kujiunga na masomo ya Sekondari Kidato cha Kwanza katika Shule za Serikali.

Idadi ya Wanafunzi waliofaulu kujiunga na Kidato cha kwanza Januari, 2023 imeongezeka kwa Wanafunzi **166,139** sawa na ongezeko la asilimia **18.30** ikilinganishwa na Wanafunzi **907,802** waliopata alama za kuwawezesha kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2022. Kati ya waliofaulu na kupangiwa kujiunga na Kidato cha Kwanza wamo Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum **2,775** sawa na asilimia **0.26** ambao kati yao Wavulana ni **1,491** na Wasichana **1,284**.

**Ndugu Wanahabari;**

Mwaka huu kwa mara ya tatu, Uchaguzi wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza umefanyika kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Uchaguzi wa Wanafunzi (*Students Selection-Management Information System*) ulioundwa na wataalam wa TEHAMA wa **Ofisi ya Rais TAMISEMI** na **Baraza la Mitihani la Tanzania**. Mfumo huu umesaidia mambo yafuatayo:

a) Kupunguza muda unaotumika kwenye Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kujiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza;

b) Kupunguza gharama zinazotumika wakati wa Zoezi la Uchaguzi na Upangaji wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza; na

c) Kuongeza ufanisi na uwazi katika uchaguzi wa Wanafunzi kwa maana ya kuwa kila Mwanafunzi anapangwa kwenye Shule kulingana na Mwongozo wa Uchaguzi unavyoelekeza.

**3.0 Vigezo vilivyotumika Kuwapangia Shule Wanafunzi**

**Ndugu Wanahabari;**

Uchaguzi wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2023 umezingatia kigezo cha ufaulu wa mtahiniwa anayechaguliwa. Kila mtahiniwa aliyefanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka, 2022 na kupata jumla ya alama za ufaulu kati ya **121** hadi **300** amechaguliwa na kupangiwa Shule ya Sekondari ya Serikali.

Shule za Sekondari za Serikali walizopangiwa wanafunzi ziko katika makundi makuu mawili: **Shule za Bweni** na **Shule za Kutwa**. Kwa upande wa shule za bweni, shule hizi zimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni Sekondari za Bweni za Wanafunzi **wenye ufaulu wa Juu Zaidi (Special Schools),** Shule za **Sekondari za bweni - Ufundi** na shule za Sekondari za **Bweni Kawaida**. Shule za Bweni ni za Kitaifa na hivyo, zimepangiwa kupokea Wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kwa kuzingatia mgawanyo wa nafasi uliobainishwa na vigezo vilivyowekwa ili kuimarisha Utaifa.

**Ndugu Wanahabari;**

Jumla ya Shule za Sekondari **4,309** zimepangiwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, kati ya hizo Shule **38** sawa na asilimia **0.88** ni shule za bweni za kitaifa na Shule **4,271** sawa na asilimia **99.12** ni shule za kutwa. Uchaguzi

wa Wanafunzi katika makundi hayo ulifanyika kwa mujibu wa Mwongozo wa Uchaguzi kama ifuatavyo:

a) **Shule za Sekondari za Bweni kwa Wanafunzi wenye Ufaulu mzuri zaidi**

Nafasi katika Shule za Wanafunzi wenye Ufaulu mzuri zaidi zimegawanywa kwa kila Mkoa kulingana na idadi ya watahiniwa wa Darasa la Saba waliosajiliwa katika Mkoa husika kwa kutumia Kanuni ya kugawa nafasi hizo Kitaifa. Nafasi zilizotolewa kwa Mkoa zimegawanywa sawa kwa kila Halmashauri zilizopo katika Mkoa husika. Shule hizi zipo saba (7) ambazo ni **Msalato, Mzumbe, Kilakala, Kibaha, Ilboru, Tabora Wasichana** na **Tabora Wavulana**.

b) **Shule za Sekondari za Bweni Ufundi**

Nafasi katika Shule za Sekondari za Ufundi zimegawanywa kwa kila Mkoa kulingana na idadi ya watahiniwa wa Darasa la Saba waliosajiliwa kwa Mkoa husika kwa kutumia Kanuni ya kugawa nafasi hizo Kitaifa. Nafasi zilizotolewa kwa Mkoa zimegawanywa sawa kwa kila Halmashauri za Mkoa husika. Shule za Sekondari za Bweni za Ufundi zipo tisa ambazo ni **Tanga Tech, Moshi Tech, Musoma Tech, Bwiru Tech, Ifunda Tech, Iyunga Tech, Mtwara Tech, Mwadui Tech** na **Chato Tech**.

c) **Shule za Sekondari za Bweni Kawaida**

Nafasi katika Shule za Bweni **22** za Kawaida za Kitaifa zimegawanywa kwa kila Halmashauri kwa kufuata idadi ya watahiniwa wa Darasa la Saba waliotoka katika Halmashauri za Wilaya na wanaotoka katika mazingira magumu pekee kwa kutumia Kanuni ya kugawa nafasi hizo Kitaifa. Katika kundi hilo, Wanafunzi kutoka Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji hawakuhusishwa isipokuwa kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

**Ndugu wanahabari;**

Ninapenda kusisitiza kuwa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule za Bweni ni wachache sana na hutegemea Idadi inayotengwa kwa kila Mkoa/Halmashauri. Orodha ya wanafunzi katika Halmashauri hupangwa kulingana na ufaulu wao kwa jinsi (order of merit) na waliofaulu Zaidi hupangwa shule za bweni kulingana na nafasi zilizopo kwenye Halmashauri husika. Kwa msingi huo, sio kila mwanafunzi anayefaulu kwa wastani wa A anaweza kuchaguliwa shule ya bweni. Nimeona nisisitize hili ili kupata uelewa wa pamoja hususan kwa wazazi/walezi na wanafunzi ambao hudhani kwamba mwanafunzi kupata wastani wa A ndicho kigezo pekee cha kuchaguliwa kujiunga na shule za Bweni.

**Ndugu Wanahabari,**

Kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa hapo juu, Wanafunzi **4,224** sawa na asilimia **0.39** wamechaguliwa kujiunga na Shule za Bweni za Kitaifa, kwa mchanganuo ufuatao:

(i) Wanafunzi **932** (Wavulana **512** na Wasichana **420**) sawa na asilimia **0.09** wamechaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za Wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi;

(ii) Wanafunzi **1,323** (Wavulana **1,110** na Wasichana **213**) sawa na asilimia **0.12** wamechaguliwa kwenda Shule za Sekondari za Ufundi;

(iii) Wanafunzi **1,969** (Wavulana **979** na Wasichana **990**) sawa na asilimia **0.18** wamechaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za Bweni Kawaida: na

(iv) Wanafunzi **1,069,717** (Wavulana **512,245** na Wasichana **557,472**) sawa na asilimia **99.61** wamechaguliwa kwenda Shule za Sekondari za Kutwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**Ndugu Wanahabari;**

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilifanya maandalizi mapema ili kuhakikisha kuwa

wanafunzi wote watakaofaulu Mtihani wa kumaliza Darasa la Saba mwaka, 2022 wanajiunga na Elimu ya Sekondari ifikapo Januari, 2023. Kutokana na maandalizi hayo Wanafunzi wote **1,073,941** waliofaulu Mtihani wa Darasa la Saba nchini mwaka 2022 wataanza masomo yao siku moja mara muhula wa masomo utakapoanza. ***Na katika hatua hii nawataarifu kuwa muhula wa masomo kwa Shule za Msingi na Sekondari zinazomilikiwa na Serikali kwa mwaka 2023 utaanza tarehe 09 Januari 2023 kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa kalenda ya mihula uliotolewa na Kamishna wa Elimu tarehe 1 Desemba,2022.***

**Ndugu Wanahabari;**

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2023. Aidha, nawashukuru Walimu, Wakuu wa Shule, Kamati za Shule, Maafisa Elimu Kata, Maafisa Elimu wa Halmashauri na Mikoa pamoja na Viongozi wote wa Halmashauri na Mikoa na Wadau wa Elimu nchini kwa kutoa ushirikiano katika kusimamia uendeshaji na utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini.

Aidha, napenda kuwaasa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza mwaka 2023 katika Shule za Sekondari za Serikali nchini, watumie vizuri fursa waliyoipata kusoma kwa bidii ili wafikie malengo waliyojiwekea.

## 4.0 Maelekezo ya Mheshimiwa Waziri

**Ndugu Wanahabari;**

Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kuhakikisha kuwa:

(a) **Wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo yao mwezi 9 Januari, 2023 bila vikwazo vya aina yoyote** ili kutekeleza azma ya Serikali ya utoaji wa Elimumsingi. Jambo hili litafanikiwa endapo kila mmoja kwa nafasi yake atawajibika katika kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea hivi sasa ili uweze kukamilika kwa wakati kama tulivyojipangia. Hivyo, Ninawaagiza Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha maandalizi yote ikiwemo ujenzi wa miundombinu yote kwa ajili ya kuwapokea Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mwaka, 2023 inakamilika kabla au ifikapo tarehe 24 Desemba 2022.

(b) Wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni wanaripoti shuleni ifikapo tarehe **07 Januari, 2023**; na kwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na shule za kutwa wanaripoti shuleni ifikapo tarehe **09 Januari, 2023**. Wazazi/Walezi na Jamii wanahimizwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya, Halmashauri na Shule ili kuhakikisha

kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa wanaandikishwa, wanahudhuria na kubakia Shuleni hadi watakapohitimu Elimu ya Sekondari.

**(c)** Waheshimiwa **Wakuu wa Mikoa** na **Wakuu wa Wilaya**, Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kusimamia uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali na Msingi na kuhakikisha uandikishwaji huo unakamilishwa ifikapo tarehe **31 Disemba 2022**. Ufanisi katika zoezi la uandikishwaji kukamilishwa kwa wakati litasaidia Watoto wetu kuanza kusoma tarehe **9 Januari 2023** siku shule zitakapofunguliwa.

**Ndugu Wanahabari;**

Orodha ya Wanafunzi wote waliochaguliwa pamoja na Fomu za Maelezo ya Kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2023 (*Joining Instructions)* kwa Shule zote za Bweni za Kitaifa zinapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia kiunganishi cha ***www.tamisemi.go.tz*** na Baraza la Mitihani la Tanzania ***www.necta.go.tz.***

**Ndugu Wanahabari;**

Pamoja na maelekezo haya, kwa Mwanafunzi, Mzazi/Mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelekezo au ufafanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri au apige simu kwenye Kituo cha Huduma kwa Wateja, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa namba za simu **026 2160210** au **0735 160210**.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**

Angellah J. Kairuki, (Mb)

**WAZIRI WA NCHI, OR - TAMISEMI**

14 Disemba, 2022



CamScanner